Baraza la Famasi Tanzania

# KITINI CHA JINSI YA KUTUMIA MFUMO WA SIMU YA KIGANJANI KATI YA BARAZA LA FAMASI NA WAMILIKI WA MADUKA NA WATAALAMU WA DAWA




SDSI Sustainable Drug Seller Initiatives

A CATALYST FOR INNOVATION

**YALIYOMO**

UTANGULIZI ...... 3

SEHEMU YA KWANZA: MALIPO YA KUHUISHA VIBALI ...... 4

1.1 MALIPO YA KUHUISHA VIBALI NA LESENI ...... 4

Taratibu za malipo ya kuhuisha vibali na leseni – Fig 1.0 ...... 5

1.2 UTHIBITISHO WA MALIPO ...... 6

Muundo wa ujumbe mfupi wa maandishi ...... 6

1.3. UJUMBE WA KUKUMBUSHA KWA AJILI YA MALIPO MBALIMBALI ...... 6

Muundo wa ujumbe mfupi wa maandishi wa ukumbusho kwa wanataaluma ...... 6

Muundo wa ujumbe mfupi wa maandishi wa ukumbusho kwa wamiliki wa maduka ...... 6

1.4. ORODHA YA WADAIWA ...... 7

Muundo wa ujumbe huu ni kama ifuatavyo ...... 7

SEHEMU YA PILI: RIPOTI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KWENYE DUKA LA DAWA ...... 7

Muundo wa Ujumbe ...... 8

1.5. HATUA ZA KUTUMA RIPOTI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA DUKA LA DAWA KWENDA BARAZA ...... 8

Utaratibu wa kutoa ripoti ya huduma zinazotolewa kwenye duka la dawa – Fig 2 ...... 9

SEHEMU YA TATU: HUDUMA ZA ZIADA ZINAZOPATIKANA KWA NJIA YA SIMU ...... 10

1.6. HATUA ZA KUFUATA ILI KUPATA HUDUMA ZA ZIADA ZINAZOPATIKANA KWA NJIA YA SIMU KUTOKA BARAZA LA FAMASI ...... 11

Huduma za ziada zinazopatikana kwa njia ya Simu – Fig 3 ...... 12

SEHEMU YA NNE: HUDUMA KWA WATEJA KUPITIA BARUA PEPE NA UJUMBE MFUPI ...... 12

Huduma kwa wateja kupitia barua pepe na ujumbe mfupi – Fig 4 ...... 13

BARAZA LA FAMASIA TANZANIA

# Mwongozo kwa Mtumiaji

---

# MFUMO WA SIMU YA KIGANJANI KATI YA BARAZA LA FAMASI NA WAMILIKI WA MADUKA NA WATAALAMU WA DAWA

© Pharmacy Council of Tanzania
External Mabibo, Mandela Road/TFDA
Dar Es Salaam, Tanzania
Phone +255 22-245 1007 • Email msajili@pharmacycouncil.go.tz

## UTANGULIZI

Baraza la Famasi ni taasisi iliyoundwa chini ya Sheria ya Famasi Na. 1 ya mwaka 2011. Baraza hili limeundwa kwa madhumuni ya kulinda na kusimamia taaluma ya Famasi na kazi zake, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa katika vituo vya tiba na maduka ya dawa zinaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowekwa.

Baraza la Famasi kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Management Sciences for Health (MSH) na shirika la Invention and Technological Ideas Development Organization (ITIDO) limeweza kutengeneza mfumo wa ukusanyaji na utunzaji wa taarifa (Database) ambao utarahisisha utendaji wa kazi wa Baraza. Mfumo wa matumizi ya simu ya kiganjani ni sehemu mojawapo ya mifumo mbalimbali inayosaidia kuboresha ukusanyaji na utunzaji wa taarifa.

Kwa kupitia teknolojia ya mawasiliano ya simu ya kiganjani huduma mbalimbali zitakazotolewa ni kama zifuatavyo;

- Malipo ya kuhuisha vibali
- Ripoti za huduma zinazotolewa kwenye Duka la Dawa
- Huduma za ziada zinazopatikana kwa njia ya simu
- Kutoa taarifa mbalimbali katika sekta ya dawa kwa wadau(alerts)
- Taarifa za mrejesho (feedback reports)
- Huduma kwa wateja kwa ujumbe (web and sms help line)

Lengo la kitini hiki ni kumwezesha mtumiaji kuelewa na kuutumia kwa urahisi huduma zinazopatikana kwa njia ya simu ya kiganjani zinazotolewa na Baraza la Famasi.

Kitini hiki kimegawanyika katika sehemu kuu nne

1. Sehemu ya Kwanza : Malipo ya kuhuisha vibali
2. Sehemu ya pili: Ripoti za huduma zinazotolewa kwenye Duka la Dawa
3. Sehemu ya tatu: Huduma za ziada zinazopatikana kwa njia ya simu
4. Sehemu ya nne: Huduma kwa wateja kwa ujumbe (web and sms help line).

## SEHEMU YA KWANZA: MALIPO YA KUHUISHA VIBALI

Sehemu hii inafafanua kuhusu taarifa ambazo Baraza la Famasi lingependa kuziwasilisha kwa wamiliki wa maduka la dawa, wataalamu wa dawa na watoa huduma katika maduka ya dawa. Taarifa hizi zinajumuisha taarifa za malipo ya vibali na leseni (malipo mapya, kuhuisha vibali na leseni, usajili wanataaluma, na uthibitisho wa malipo, malipo ya adhabu (penalties), orodha ya wadaiwa.

### 1.1 MALIPO YA KUHUISHA VIBALI NA LESENI

Haya ni malipo yanayofanywa kila ifikapo mwisho wa mwaka ambapo wamiliki wa maduka ya dawa wanatakiwa kuhuisha vibali na wataalamu wa fani ya famasi wanahitajika kuhuisha leseni. Ili kufanikisha hilo zifuatazo ni hatua ambazo mtumiaji anapaswa kuzifuata katika kuhuisha vibali au leseni. Mfumo utakaotumika kwa sasa ni kutumia mfumo wa M-Pesa kupitia simu ya kiganjani. Malipo ya kuhuisha vibali yafanywe kabla ya tarehe 30 – Juni ya kila mwaka na malipo ya leseni za wanataaluma yafanyike kabla ya tarehe 31 – Disemba ya kila mwaka. Endapo malipo hayatofanyika kwa wakati mhusika atalazimika kulipa kiasi anachodaiwa pamoja na faini ya asilimia 25 ya malipo halisi. Maelezo ya jinsi ya kufahamu kiasi cha malipo yanapatikana katika sehemu ya 3 ya kitini hiki.

**Hatua:**

1. Unapaswa kutumia laini (simcard) ya mtandao wa Vodacom iliyosajiliwa kwenye huduma ya M-Pesa
2. Piga *150*00#
3. Fuata maelekezo ya mfumo wa M-pesa kwa kiswahili
4. Chagua - Lipa kwa Mpesa
5. Chagua - weka namba ya kampuni
6. Tafadhali weka namba ya kampuni ((eg. 900800)
7. Weka namba ya kumbukumbu ya malipo (FIN au PIN)
8. Weka kiasi
9. Ingiza namba ya siri
10. Bonyeza 1 kuthibitisha au 2 kubatilisha

**ANGALIZO**

Kama utakuwa umekamilisha muamala vizuri, utapokea ujumbe mfupi wa kuthibitisha malipo na namba ya risiti ya malipo na pia utapokea ujumbe mfupi kutoka Baraza la Famasi.

**Taratibu za malipo ya kuhuisha vibali na leseni – Fig 1.0**

**1** Piga *150*00##

> *150*00#

**2** Chagua Lipa Kwa Mpesa

> Lipa Bili

**3** Chagua weka Namba ya kampuni

> Chagua Sehemu ya "business payment"

**4** Ingiza Namba ya kampuni (e.g.900800)

> Ingiza namba ya kampuni

**5** Weka Namba ya kumbukumbu ya malipo (FIN au PIN)

> Ingiza namba ya kumbukumbu

**6** Weka Kiasi

> Ingiza kiasi unacho lipa

**7** Ingiza Namba ya Siri

> Ingiza namba ya Siri

**8** Bonyeza 1.Kuthibitisha au 2. Kubatilisha

> Ingiza 1.Kuthibitisha au 2. Kubatilisha

**9** utapokea ujumbe mfupi wa kuthibitisha malipo na namba ya risiti ya malipo na pia utapokea ujumbe mfupi kutoka Baraza la Famasi

> 02001 confirmed Tsh. 50,000 sent to account 04088162402 on 25/1/2014 at 8:24PM.

## 1.2 UTHIBITISHO WA MALIPO

Mara baada ya kufanya malipo husika ujumbe mfupi wa uthibitisho utatumwa kupitia namba ya simu iliyotumika kufanya malipo.

**Muundo wa ujumbe mfupi wa maandishi**

| |
|---|
| Imepokelewa <kiasi> toka kwa<jina>namba ya utambulisho<PIN/FIN> kwa ajili ya <aina ya malipo>. Uthibitisho wa muamala < uthibitisho wa muamala><br><br>**Mfano:** Imepokelewa < 75,000>kutoka<jina>namba ya utambulisho <2010202020> kwa ajili ya <renewal fee> uthibitisho wa muamala. |

## 1.3. UJUMBE WA KUKUMBUSHA KWA AJILI YA MALIPO MBALIMBALI

Huu ni ujumbe mfupi wa maandishi unaotumwa na Baraza la Famasi kupitia simu ya kiganjani kwa wataalamu na wamiliki wa maduka ya dawa kama njia ya kuwakumbusha kufanya malipo yao kwa wakati.

**Muundo wa ujumbe mfupi wa maandishi wa ukumbusho kwa wanataaluma**

| |
|---|
| Tafadhali lipa < aina ya malipo> ya mwaka <kipindi cha malipo> kabla ya tarehe <tarehe husika>. Kumbuka usipolipa kwa wakati, utalazimika kulipa malipo ya ziada kama adhabu.<br><br>**Mfano:** Tafadhali lipa <malipo ya kuhuisha usajili wako>ya mwaka<2015> kabla ya tarehe<31-Disemba 2014>Kumbuka, usipolipa kwa wakati, utalazimika kulipa malipo ya ziada kama adhabu. |

**Muundo wa ujumbe mfupi wa maandishi wa ukumbusho kwa wamiliki wa maduka**

| |
|---|
| Tafadhali lipa < aina ya malipo> kwa mwaka <kipindi cha malipo> kabla ya tarehe <tarehe husika>. Kumbuka usipolipa kwa wakati, utalazimika kulipa malipo ya ziada kama adhabu..<br><br>**Mfano:** Tafadhali lipa <malipo ya kuhuisha usajili wako>ya mwaka<2015> kabla ya tarehe<31-Disemba 2014>Kumbuka, usipolipa kwa wakati, utalazimika kulipa malipo ya ziada kama adhabu. |

### 1.4. ORODHA YA WADAIWA

Mfumo huu utatengeneza orodha ya maduka na wataalamu wanaodaiwa na kisha kutuma ujumbe mfupi kwa mratibu wa Barazawa kanda husika.

**Muundo wa ujumbe huu ni kama ifuatavyo**

> Orodha ya maduka ambayo yanahitajika kulipia ada ya kuhuisha usajili
>
> 1. Duka la dawa 1 <Namba ya Utambuzi, Jina la Duka, Kiasi kinachodaiwa>
> 2. Duka la dawa 2 <Namba ya Utambuzi, Jina la Duka, Kiasi kinachodaiwa>
> 3. Duka la dawa 3 <Namba ya Utambuzi, Jina la Duka, Kiasi kinachodaiwa>

## SEHEMU YA PILI: RIPOTI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KWENYE DUKA LA DAWA

Hizi ni ripoti zitakazotumwa kwa njia ya ujumbe mfupi wa maandishi ambazo watoa dawa wanatuma kwenda Baraza la Famasi kupitia simu ya kiganjani. Ripoti hizi zitakuwa katika muundo ufuatao:

Vifuatavyo ni vifupisho vya maneno yatakayotumika wakati wa kutuma ripoti ya huduma zinazotolewa kwenye duka la dawa.

| KIFUPISHO | MAELEZO |
|---|---|
| 1. FIN | Namba ya utambulisho wa duka la dawa |
| 2. PIN | Namba ya utambulisho ya mwanataaluma wa Famasi |
| 3. RP | Kipindi cha taarifa |
| 4. A | Idadi ya wagonjwa |
| 5. B | Idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano |
| 6. C | Idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wenye malaria |
| 7. D | Idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano waliopata rufaa kwenda kituo cha tiba |
| 8. E | Idadi ya wanawake waliopokea vidonge vya uzazi wa mpango |
| 9. F | Idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano wenye ugonjwa wa kuharisha |

**Muundo wa Ujumbe**

| |
|---|
| Namba ya utambulisho <FIN>, Kipindi cha taarifa <Kipindi husika > Alama za utambuzi1 < Alama husika na Idadi> …………….Alama za utambuzin <Alama husika na Idadin>. |

**MUHIMU:**
Wakati wa kutuma ujumbe zingatia sana muundo husika wa ujumbe vinginevyo ripoti itakayotumwa haitapokelewa.

**MFANO:**
Ufuatao ni mfano wa ripoti itakayotumwa kwenda Baraza kutoka katika Maduka ya dawa kwa kipindi husika cha kutolea taarifa

| KIFUPISHO CHA KIASHIRIA | NAMBA/IDADI |
|---|---|
| 1. FIN | 01010400003 |
| 2. RP | 06 |
| 3. B | 13 |
| 4. C | 15 |
| 5. D | 4 |
| 6. E | 35 |
| 7. A | 8 |
| 8. F | 16 |

Ripoti hii ya mfano itatumwa kama ujumbe mfupi wa maandishi kupitia simu ikiwa na muundo ufuatao:-

| |
|---|
| **FIN**01010400003 **RP**6 **A**8 **B**13 **C**15 **D**4 **E**35 **F**16 |

## 1.5. HATUA ZA KUTUMA RIPOTI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA DUKA LA DAWA KWENDA BARAZA


1. Fungua sehemu ya "menu" kwenye simu yako
2. Chagua sehemu ya ujumbe mfupi (message)
3. Chagua sehemu ya kuandika ujumbe
4. Ingiza ripoti kwenye muundo sahihi. Mfano; FIN01010400003 RP1 B5 C6. Hakikisha umeacha nafasi kati ya kifupisho na idadi/namba
5. Tuma ujumbe wako kwenda namba ………kama ilivyoaninishwa kwenye michoro hapo chini.

**ZINGATIA:**
Ukishatuma taarifa taarifa yako, utapata ujumbe mfupi wa mrejesho kutoka Baraza la Famasi.

Zifuatazo ni aina za ujumbe wa mrejesho

| TAARIFA | UJUMBE WA MREJESHO |
|---|---|
| 1. Iwapo ujumbe umefanikiwa kutumwa kikamilifu | Ahsante, Ujumbe umepokelewa kutoka kwenye Duka FIN: 01010400003 Kipindi cha kutoa taarifa:….. tarehe ya kutuma: ………… |
| 2. Iwapo muundo wa ujumbe sio sahihi | Samahani, Muundo wa ujumbe sio sahihi tafadhali rekebisha kisha utume tena |
| 3. Iwapo muundo wa ujumbe ni sahihi ila moja kati ya vifupisho vilivyotumika si sahihi. Mfano FN badala ya FIN | Muundo wa ujumbe ni sahihi isipokuwa FN sio kifupisho sahihi |
| 4. Iwapo muundo wa ujumbe ni sahihi isipokuwa FIN/PIN ilkiyotumika haitambuliki. mfano FIN: 098889 badala ya 01010400003 | Muundo wa ujumbe ni sahihi isipokuwa FIN:098889 haitambuliki |

**Utaratibu wa kutoa ripoti ya huduma zinazotolewa kwenye duka la dawa – Fig 2**



## SEHEMU YA TATU: HUDUMA ZA ZIADA ZINAZOPATIKANA KWA NJIA YA SIMU

Hizi ni huduma ambazo wateja wanaweza kuzipata kutoka Baraza la Famasi. Kwa mfano, mteja angependa kujua vigezo vya kuzingatia wakati wa kuanzisha duka la dawa, taratibu za usajili wa duka la dawa n.k. Ili kupata huduma hizo mteja atahitajika kutuma neno/herufi maalumu kwa kupitia ujumbe mfupi wa maandishi kwenye namba itakayotolewa na Baraza.

Ifuatayo ni orodha ya maneno/ herufi zinazoweza kutumika kupata huduma za ziada zinazopatikana kwa njia ya simu

| NENO/HERUFI | MAELEZO |
|---|---|
| **1. P** | P<Addo/Famasi>Kupata taarifa kutoka Baraza la Famasi kuhusu utaratibu wa kuanzisha duka la dawa |
| **2. PH** | Kupata taarifa kutoka Baraza kuhusu taratibu za usajili wa mfamasia |
| **3. RF** | RF<PIN> Kupata taarifa kutoka Baraza kuhusu kiasi cha malipo anachodaiwa mtaalamu ili kuhuisha leseni yake |
| **4. RF** | RF<FIN> Kupata taarifa kutoka Baraza kuhusu kiasi cha malipo mmiliki wa duka la dawa anachodaiwa ili kuhuisha kibali/leseni |
| **5. PF** | Kupata taarifa kuhusu kiasi cha malipo mmiliki wa Famasi anachotakiwa kulipia kwa ajili ya kufanya taaluma ya famasi. |
| **6. PA** | PA <PIN> = Kupata taarifa kutoka Baraza ili kuweza kujua kama Mfamasia au mtoa dawa fulani yupo huru au anasimamia duka jingine<br><br>PA <Personnel Category code> = Kupata taarifa za upatikanaji wa mwanataaluma ambao hawasimamii maduka kwa wakati huo kwenye kundi husika<br><br>NB: Hii itaanza na taarifa za wafamasia |
| **7. REG** | REG<PIN/FIN> = Kupata taarifa kuhusu usajili wa mwanataaluma/duka husika |
| **8. MA** | Kupata ratiba na upatikanaji wa mafunzo ya ADDO |
| **9. RT** | RT<FIN> = Kupata taarifa juu ya vyuo vilivyosajiliwa na Baraza la Famasi |
| **10. ED** | ED<forensic exam> = Kupata taarifa juu ya tarehe ya kufanya mtihani wa forensic<br>ED<certificate exam> = Kupata taarifa juu ya tarehe ya kufanya mtihani wa ngazi ya cheti |
| **11. ER** | ER<Temp PIN/exam number>Kupata taarifa juu ya matokeo ya mtihani |
| **12. NR** | NR<Temp FIN/PIN> = kupata taarifa juu ya maendeleo ya usajili wa duka jipya/Mfamasia mpya |

## 1.6. HATUA ZA KUFUATA ILI KUPATA HUDUMA ZA ZIADA ZINAZOPATIKANA KWA NJIA YA SIMU KUTOKA BARAZA LA FAMASI

1. Fungua sehemu ya “menu” kwenye simu yako
2. Chagua sehemu ya ujumbe
3. Chagua sehemu ya kuandika ujumbe
4. Ingiza neno/herufi maalumu kwa ajili ya huduma unayotaka kupata taarifa zake (kwa mfano P kwa ajili ya taarifa ya vigezo vya kuanzisha duka la dawa na PR kwa ajili ya taarifa za taratibu za kusajili duka la dawa
5. Bonyeza “option”
6. Chagua “send”
7. Utaulizwa namba ya simu. Ingiza ………..
8. Chagua “OK” kutuma ujumbe

**ANGALIZO:**


Ukisha tuma ujumbe mfupi wa maneno utapata taarifa fupi kutoka Baraza la Famasi

Zifuatazo ni aina za ujumbe mfupi wa maneno utakazotegemea kutumiwa :-

A. Kama neno/herufi P imeandikwa sawasawa; utapokea ujumbe ufuatao For Pharmacy: Kwa Famasi
B. Insert correct content (Weka ujumbe sahihi)
C. Iwapo neno/herufi limekosewa na kuandikwa “K” badala ya “P” tegemea kupata ujumbe ufuatao
D. K: si neno/herufi sahihi

DUKA LA DAWA MUHIMU

**Huduma za ziada zinazopatikana kwa njia ya Simu – Fig 3**




## SEHEMU YA NNE: HUDUMA KWA WATEJA KUPITIA BARUA PEPE NA UJUMBE MFUPI

Hii ni moja kati ya huduma zilizopo kwenye mfumo wa huduma wa simu ya kiganjani wa Baraza la Famasi .Mteja anaruhusiwa kuuliza taarifa yoyote kuhusu utendaji kazi na huduma zinazotolewa na Baraza. Maombi yatatumwa kwa kufuata mfumo maalumu wa ujumbe mfupi wa maandishi kwenda Baraza unaoweza kutumwa kwa njia ya simu au barua pepe. Ujumbe huu utaanza na neno "Msaada" ukifuatiwa na ujumbe husika.

**MFANO:** <**msaada** > nafasi<**ujumbe husika**>

**ANGALIZO:**
Ukisha tuma ujumbe mfupi wa maneno utapata taarifa fupi kutoka Baraza la Famasi.

Hatua za kutuma ujumbe/msaada kwa njia ya simu ya kiganjani

1. Fungua sehemu ya  menu kwenye simu yako
2. Chagua sehemu ya ujumbe
3. Chagua sehemu ya kuandika ujumbe
4. Ingiza ujumbe sahihi.
   **MFANO:**
   **Msaada ningependa kufahamishwa mafunzo ya watoa dawa kwa sasa yanafanyika wapi?**
5. Chagua sehemu ya “Option”
6. chagua “select”
7. chagua “send”
8. Utaulizwa namba ya simu,
9. Ingiza …………
10. Chagua “OK” ili kutuma ujumbe

Ukisha tuma, utapata ujumbe mfupi wa maneno kutoka Baraza la Famasia. Kama neno ulilotuma  ni “Msaada” utakaopokelewa ujumbe unaosema  “ Asante, tumepokea maombi yako, tunayafanyia kazi”.
Aina zifuatazo  za ujumbe mfupi wa maneno zinategemewa kutumwa kama mrejesho;

| CASE | MESSAGE RECEIVED |
|---|---|
| 1. Ujumbe umetumwa kikamilifu | Asante, tumepokea maombi yako, tunayafanyia kazi |
| 2. Kama neno ulilotuma limekosewa kwaMfano “hope” badala ya “help” au “msaada” | Samahani, hope si neno sahihi tafadhali rekebisha na utume tena |

**Huduma kwa wateja kupitia barua pepe na ujumbe mfupi – Fig 4**





